Nuru ya Kiswahili, Juzuu 3(1), Juni 2024: 1-26
DOI: https://doi.org/10.58548/2024nuru31.0126

# Matumizi ya Fantasia katika Usanaji wa Filamu za Kiswahili Nchini Tanzania

**Gervas A. Kasiga**
**Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Dodoma**
gervas.kasiga@udom.ac.tz

**Ikisiri**

Makala hii inahusu matumizi ya fantasia katika usanaji wa filamu za Kiswahili nchini Tanzania. Fantasia ni miongoni mwa vipengele vinavyohusishwa na uhalisiajabu ambavyo hutumiwa na watunzi kusana kazi zao. Utafiti uliozaa makala hii ulitumia mbinu za kitaamuli. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za uchambuzi matini na mahojiano. Filamu teule zilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Uchambuzi wa data za makala umefanyika kwa kutumia Nadharia ya Fantasia. Filamu za Kiswahili za Kitanzania za *Jamila na Pete ya Ajabu* na *Nsyuka* zimetumika kama sampuli ya kubainisha mdhihiriko wa fantasia. Maeneo ambayo ufantasia umejitokeza katika filamu teule yamebainishwa. Maeneo hayo yamehusisha matukio ya kihadithi ya filamu pamoja na uwasilishaji wa ujumbe kupitia uigizaji. Aidha, ilibainika kuwa fantasia hutumika katika kuunda filamu kwa malengo ya ujengaji wa taharuki, ubunifu, na usisimuaji wa hisia ya mtazamaji. Vilevile, ilibainika kuwa matumizi ya fantasia katika filamu teule yana tija na madhara kwa usanaji na uwasilishaji wa filamu za Kiswahili kwa hadhira. Kufuatia matokeo haya, inapendekezwa watayarishaji wa filamu kuzingatia uwiano wa matumizi ya fantasia katika filamu ili kuepusha madhara yaliyoelezwa katika makala hii.

**Dhana za Msingi:** Fantasia, usanaji, na filamu

## Utangulizi

Usanaji wa kazi za fasihi huhusisha mbinu anuwai za kifani. Mathalani, mbinu za matumizi ya lugha, mtindo, muundo, na uundaji wa wahusika kisilika hutumika katika kusana kazi za fasihi (Walibora, 2010; Yangi, 2015; Hamad, 2019; Ponera & Kasiga, 2019; Kasiga & Maffa, 2021). Kimsingi, mbinu hizo huwa na dhima kubwa ya kuifanya kazi ya fasihi kuwa na mvuto kwa wasikilizaji, wasomaji, na watazamaji wake. Katika kazi ya fasihi, mvuto husaidia hadhira kujikita kufuatilia simulizi ya hadithi kwa umakini na kupata ujumbe wake. Ufuatiliaji huo wa simulizi huiwezesha hadhira kuyapokea kikamilifu maudhui yaliyomo ndani ya kazi ya fasihi. Hivyo basi, kimantiki, kufika kwa ujumbe uliokusudiwa kwa namna bora ni mafanikio makubwa kwa msanii wa kazi ya kifasihi na sanaa kwa upana wake.

Fantasia ni kati ya mbinu za kifani zinazotumiwa na wasanii kujenga maudhui ya kazi zao. Fantasia ni hali ya uajabuajabu au undoto-ndoto unaotamalaki ndani ya kazi ya fasihi. Aghalabu, undoto-ndoto huo husheheni mambo ya ajabu na, wakati mwingine, ya kuogopesha na kutisha. Kwa mfano, kazi zinazojengwa kifantasia hutumia wahusika kama vile vinyamkera, mizimu, majitu ya kutisha, na wafu. Mara zote, wahusika hao hutumia nguvu zisizomithilika katika maisha ya kawaida ya kibinadamu (Hunt, 1990; Sadner, 1996). Mambo yanayobebwa kifantasia huwa vigumu kushuhudiwa katika ulimwengu halisi (Wamitila, 2013). Katika ulimwengu wa sanaa na fasihi, mambo hayo hupambanuliwa ili kuweza kukidhi matakwa ya kisanii wakati wa uwasilishaji wa kazi husika ya kifasihi (Bakize, 2012). Kwa mintarafu hiyo, uhakiki wa kidhima na kifani wa kazi ya fasihi kupitia fantasia huchanganuliwa kupitia ishara zote zilizotumiwa

na mtunzi wa kazi husika ya fasihi (Cragan & John, 1995; Mutua & Furaha, 2014). Kwa hoja hiyo, makala hii inatafsiri ishara zilizoibuliwa na fantasia na kuzitolea ufafanuzi wa kimaelezo kwa kuzingatia dhima yake katika usanaji wa filamu.

Uga wa filamu za Kiswahili uliteuliwa kumakinikiwa kwa sababu ni uwanja mpya wa kifasihi unaokua kwa kasi na kushika hadhira kubwa ya wazungumzaji wa Kiswahili wa Afrika Mashariki na nchi jirani (Suwed, 2013; Kasiga, 2018). Vilevile, hivi sasa, filamu za Kiswahili zimebainika kuchukua nafasi kubwa katika kuitangaza lugha ya Kiswahili na utamaduni mpana wa Watanzania (Kasiga, 2013). Filamu imetokana na maendeleo makubwa ya utambaji hadithi yaliyovuka njia za kijadi. Namna hiyo mpya ya utambaji huchagizwa na ufanisi wa kiteknolojia (Mrikaria, 2007; Mahenge, 2016; Abdallah, 2018; Kasiga, 2022). Isitoshe, filamu ni fasihi simulizi iliyostawi (Kasiga & Luhwago, 2020). Kwa hali hiyo, imedhihirika kuwa filamu ni uwanja mpya wa kifasihi wenye kuhitaji kuchimbuliwa zaidi kitafiti ili kuukuza kitaaluma katika uwasilishaji wa masuala ya kijamii nchini Tanzania (Kasiga, 2024).

Hivyo, makala hii inalenga kujadili nafasi ya matumizi ya fantasia katika usanaji wa filamu za Kiswahili kwa kuakisi mambo matatu. Nayo ni kubainisha mdhihiriko wa fantasia kupitia filamu teule, kujadili sababu za kutumia fantasia katika filamu teule, na kutathimini athari ya fantasia katika usanaji wa filamu za Kiswahili.

## Nadharia ya Fantasia

Nadharia ya Fantasia iliongoza mchakato wa uchambuzi, tathimini, na utoaji wa matokeo. Nadharia ya Fantasia imeasisiwa na Mutua na Furaha, 2014). Nadharia hii ina misingi mitatu. Msingi wa kwanza unatanabahisha

kuwa ubunifu wa kidhahania huwa na athari katika usanaji wa mandhari na uteuzi wa wahusika. Ili kuupata ujumbe uliolengwa na mtunzi kupitia msingi huu, ni muhimu kumakinia dhima, hisia za wahusika, pamoja na uhusika wao. Hivyo, utafiti uliozaa makala hii ulichanganua wasifu, haiba za ndani za wahusika, pamoja na mawasilisho ya maudhui yaliyojengwa kupitia matendo ya wahusika. Kupitia matendo ya wahusika hao, ilidhamiriwa kubaini ni kwa namna gani fantasia inajitokeza katika kuukamilisha ujumbe uliokusudiwa na msanii kwenda kwa hadhira yake.

Msingi wa pili unabainisha kuwa usimulizi ndani ya fantasia hupambanua wasifu wa mtu, kundi la watu, jamii au taifa (Mutua & Furaha, 2014). Msingi huu ulitumiwa kufanya uanishaji wa wahusika wa kifantasia katika filamu teule. Usawiri wa sifa na tabia zao uliwezesha kubaini umuhimu wao katika uundaji, ujitokezaji, na matumizi ya fantasia katika uwasilishaji wa filamu teule.

Msingi wa tatu unafafanua kwamba uhalisia wa kifantasia unaundwa kupitia matumizi ya ishara (Mutua & Furaha, 2014). Msingi huu ulisaidia kuchanganua mandhari na matukio ya kifantasia kama ishara za kimawasiliano katika ulimwengu halisi. Msingi huu ulituwezesha kutambua sababu za kutumiwa kwa fantasia pamoja na athari zake katika usanaji wa filamu za Kiswahili. Pia, msingi huu unafafanua kuwa maudhui ya kifantasia hujiibua kupitia misukumo ya kani baina ya uwi na wema. Misukumo hiyo ya kikani husaidia kubaini uhalisia wa ishara zilizotumika. Hivyo, katika makala hii, kani hizo zimesaidia kufafanua msuko wa kimatukio wa filamu teule. Hii ni kutokana na kuwa ruwaza ya kimatukio humwezesha msanii kujielekeza kuteua namna bora ya msuko unaofaa katika kazi yake. Kupitia msingi huu, wahusika wa filamu teule

waligawanywa katika makundi mawili: uwi na wema. Vilevile, kupitia wajibu wao waliopewa kidrama, tuliweza kubaini jinsi matendo na matukio yao ya kifantasia yalivyojenga na kukamilisha ruwaza nzima ya masimulizi ya filamu.

## Methodolojia

Makala imeegemea katika mbinu za kitaamuli. Hii ni kwa kuwa utafiti wake unahusisha fikra katika kujenga maana ya dhana mbalimbali (Ponera, 2019). Usampulishaji lengwa ulitumika kuteua watafitiwa na vitafitiwa. Filamu za *Nsyuka* na *Jamila na Pete ya Ajabu* ambazo ni chanzo kikuu cha data za makala hii zilipatikana kupitia usampulishaji lengwa. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za uchambuzi matini na mahojiano. Mbinu ya uchambuzi matini iliruhusu kutazama, kuchanganua, na kuaridhia uibukaji wa fantasia katika filamu teule. Kupitia njia ya mahojiano, zilipatikana data zilizobainisha sababu za matumizi ya fantasia katika filamu za Kiswahili.

## Mihutasari ya Filamu Teule


Kipengele hiki kinaeleza mihutasari ya filamu zilichunguzwa. Filamu zilizotolewa maelezo ni *Jamila na Pete ya Ajabu* na *Nsyuka*. Lengo la kutoa mihutasari hiyo ni kutoa picha ya jumla ya filamu teule kwa wasomaji wa makala hii.

### Muhtasari wa filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu* (2014)

Wahusika wa filamu hii ni Haji Adam, Ben Branco, Gemma Innocent, Sophia Michael, Salma Mohamed, Dabrina Msusa, Fatma Mohamed, Azizi Mohamed, Muniru Mohamed, na Fiona. Filamu inaanza kwa kumwonesha Boss Jabir akiingia kwenye gari lake na anamkuta Jamila akiwa amejificha baada ya watoto wenzake wa mtaani kutaka kumnyang’anya mkate

aliokuwa ameuokota jalalani. Anapomwuliza maswali, anagundua kuwa mtoto huyo hana wazazi. Boss Jabir anamchukua Jamila na kumpeleka nyumbani kwake. Mkewe anaonekana kumchukia sana Jamila. Anachoma madaftari yake ili asiende shuleni. Aidha, anamshurutisha kufanya kazi zote za ndani. Zaidi, anapanga kumuua Jamila. Baada ya kwenda kwa mganga, anapewa dawa ambazo anatakiwa azichimbie chini katika nyumba yake. Kazi hiyo ya kuchimba shimo anampa Jamila aifanye. Wakati wa kuchimba shimo, Jamila anaokota pete. Anaichukua na kuisafisha. Wakati anaisafisha pete hiyo, unatokea mzimu unaomwelekeza jinsi ya kuitumia. Pete hiyo inabeba maajabu mengi, ikiwamo kumsaidia kufanya kazi za nyumbani.

Kwa mara ya pili, mke wa Jabir anaenda kwa mganga ili kumuua Jamila. Mganga anamwambia achome kisu kwenye beseni. Kila anapojaribu kufanya hivyo, anaziona sura za watoto wake badala ya sura ya Jamila. Kisha, yeye (mke wa Jabir) na mganga wanaonekana wakichapwa viboko bila kumwona mtu anayewachapa. Baada ya kurudi nyumbani kwake, anamkuta mumewe amekwisharudi. Kadhia hiyo inaishia kwa mke wa Jabir pamoja na watoto wake kufukuzwa. Jamila anamchagua Sara ambaye ni binti wa kazi ili awe mama yake (aolewe na Boss Jabir). Wanaonekana wanaishi maisha mazuri, huku pete ikiendelea kuwasaidia.




Picha Na. 1: Kasha la filamu ya Jamila na Pete ya Ajabu

**Muhtasari wa filamu ya *Nsyuka* (2003)**

Wahusika wa filamu hii ni Rehema Msangule, Mwajuma Kassim, Emmanuel Kasoga, Daktari Dimoso, na Khalid Futo. Doreen anashindwa kupata mtoto kutokana na kusumbuliwa na mzimu uitwao Nsyuka. Mama Doreen anaingiwa na mzimu huo baada ya kupita katika njia ya Nsyuka ambayo alikatazwa na wenzake. Hivyo, Nsyuka anamwingia Doreen akiwa tumboni mwa mama yake. Hatimaye, Doreen anazaliwa na kukua.

Anapokuwa mtu mzima, anashindwa kupata mtoto. Baada ya Doreen kukumbwa na tatizo hilo, Moni, ambaye ni rafiki yake, anamshauri waende kwa mganga wa kijadi ili asaidiwe kupata mtoto. Wanapofika kwa mganga, anatakiwa afanye mapenzi na Nsyuka ili aweze kupata mtoto. Doreen anakataa kufanya kitendo hicho. Moni anamshauri waende kwa mganga mwingine ambaye ni mwanamke. Huko anaambiwa afanye mapenzi na Nsyuka kupitia mchumba wake aitwaye Sanjo. Doreen anaambiwa apeleke nguo za Sanjo za kulalia. Anapoleta nguo, mganga anamvuta Nsyuka, kisha anamwingiza ndani ya Sanjo na anafanya mapenzi na Doreen bila ya yeye (Sanjo) kujua. Kupitia kitendo hicho, Doreen anashika mimba. Muda wa kujifungua unapofika, Doreen anakosa uchungu. Hata hivyo, Nsyuka anamtokea na kumwambia kuwa atajifungua mtoto wa kiume. Doreen anajifungua mtoto wa kiume na kumpa jina la Masu.

Masu anapokua, anabadilika na kuwa Nsyuka. Hili linatokea baada ya Doreen kukiuka sharti alilopewa na mganga la kutovua pete aliyompatia. Doreen, Moni, na Sanjo wanakimbilia kwa mganga ili awasaidie kutokana na Masu kuwa Nsyuka. Wanapofika kwa Mganga, wanakutana na Nsyuka akiwa na Masu ambaye naye ameshabadilika na kuwa Nsyuka.




Picha Na. 2: Kasha la Filamu ya Nsyuka

**Matokeo ya Utafiti**

Sehemu hii inawasilisha matokeo ya utafiti ambayo yamegawanyika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inabainisha matukio ya kifantasia yanayodhihirika katika filamu teule. Sehemu ya pili inawasilisha sababu za kutumiwa kwa ufantasia katika filamu teule. Sehemu ya tatu inafafanua athari zinazotokana na matumizi ya ufantasia katika filamu.

**Mdhihiriko wa fantasia katika *Filamu ya Jamila na Pete na Ajabu* (2014)**

Katika filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu*, hali ya ufantasia ilibainika katika matukio yafuatayo:

Tukio la kwanza ni Jamila alipokuwa akiiosha pete baada ya kuiokota, ambapo alitokewa na mtu aliyedai kuwa mmiliki. Kiumbe huyo wa ajabu anamsihi Jamila aitumie pete hiyo vizuri bila kuitia kwenye maji. Hali hii ya ufantasia inajipambanua katika sehemu ya pili ya filamu katika dakika ya 30:26.

Tukio la pili ni baada ya Jamila kushinda na njaa kwa muda mrefu na kuamua kuiomba pete impe chai, chapati, na maandazi. Kwa hali ya ajabu, pete inamletea chakula alichokihitaji. Jambo hilo linabainika kupitia sehemu ya pili ya filamu hii katika dakika ya 32:25. Kupitia utafiti uliozaa makala hii, ilibainika kuwa hali hii inakiuka uhalisi.

Tukio la tatu la ufantansia libainika katika sehemu ambayo inamwonesha Jamila amepewa kazi za kuosha vyombo, kufua nguo, na kudeki ili asiende shuleni. Hata hivyo, kwa mara nyingine, pete inamsaidia Jamila kufanya kazi hizo; hatimaye, Jamila anafanikiwa kuhudhuria shuleni. Matukio haya ya kindoto-ndoto yanasawiri sifa na tabia za wahusika katika kudhihirisha ufantasia.

Tukio la nne la ufantansia katika filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu* linadhihirika kupitia matukio ya mfagio unaofagia pasi na kushikwa na mtu, viti vinavyojipanga vyenyewe, pamoja na nguo zinazojianika zenyewe kwenye kamba. Hili linadhihirika kupitia sehemu ya pili ya filamu katika dakika ya 35:14 hadi 34:04.

Tukio la tano lililojengwa kifantasia ni pindi Jamila anapoiomba pete impeleke shuleni na, ghafla, anajikuta yumo darasani. Tukio hili linabainika katika sehemu ya pili ya filamu katika dakika ya 41:50. Tukio hili linakiuka uhalisi katika maisha ya binadamu.

Tukio la sita lililojengwa kifantasia lilibainika kupitia tukio ambalo pete ilizima televisheni baada ya Jamila kuiomba ifanye hivyo. Hii inadhihirika katika sehemu ya pili ya filamu katika dakika ya 43:45.

Tukio la saba linalodhihirisha ufantasia ni pale pete inapomsaidia Jamila kumwonesha begi lake la shule lilipo. Pete inarudisha upya begi la shule la Jamila baada ya kuchomwa moto na mama yake mlezi. Hali hii inamshangaza mama huyo. Suala hili linadhihirika katika sehemu ya pili ndani ya dakika ya 45:40 hadi 46:09.

Tukio la nane linalodhihirisha matukio yaliyoundwa kifantasia katika filamu hii limejitokeza pindi mama mlezi wa Jamila na watoto wake wanapoenda katika Hifadhi ya Mikumi na kumwacha Jamila peke yake nyumbani. Jamila anaiomba pete imvalishe nguo nzuri na impeleke huko walikokwenda wenzake. Pete inafanya hivyo na, ghafla, Jamila anaonekana yupo Hifadhi ya Mikumi akiwa amevaa nguo, wigi, na miwani. Baada ya muda, pete inamrudisha Jamila nyumbani na kumvalisha nguo zake za kawaida. Kisha, inamsaidia kuandaa chakula kama mama yake mlezi alivyomwagiza. Katika filamu, maeneo haya yanaonekana katika sehemu ya pili ya filamu, kuanzia dakika ya 52:56 hadi 58:57.

Tukio la tisa linadhihirika kupitia pete kumwonesha Jamila matukio na sehemu zote ambazo mama yake mlezi yupo. Hivyo, Jamila, baada ya kuona mama yake ameenda kwa mganga ili kumuua, anaiambia pete kuwa beseni la mganga lioneshe sura za watoto wa mama yake mlezi na si sura yake. Kutimizwa kwa ombi hili ndiko kulikomfanya mama mlezi azione sura za watoto wake badala ya sura ya Jamila, hivyo, kushindwa kuchoma kisu katika beseni kwa kuhofia kuwaua watoto wake. Katika filamu hii,

matukio haya yanabainika ndani ya sehemu ya pili katika saa 1:09:11 na sehemu ya pili, saa 1:06:59.

Tukio la kumi la kifantansia linadhihirika kupitia pete kutoa adhabu ya bakora. Pete inaonekana kuwachapa mama mlezi wa Jamila pamoja na mganga kama inavyoagizwa na Jamila. Zaidi ya hayo, mama mlezi wa Jamila anapofika nyumbani kwake, pete inaendelea kumchapa ili aweze kusema ukweli wa yote aliyoyapanga na kuyadhamiria kwa Jamila. Hili linadhihirika katika sehemu ya pili ya filamu katika saa 1:10:16 hadi 1:10:37.

Hivyo basi, kidhati, matukio yaliyobainishwa katika filamu hii yanakiuka uhalisi wa maisha ya kibinadamu.

**Mdhihiriko wa fantasia katika filamu ya *Nsyuka* (2003)**

Katika filamu ya *Nsyuka*, fantasia imedhihirika kupitia matukio anuwai. Tukio la kwanza linamhusisha Doreen akisoma kitabu makaburini. Ghafla, vidole vinachomoka kutokea ardhini na kumkaba. Hii inaonekana katika dakika ya 35:02 ya sehemu ya tatu ya filamu hii. Hali hiyo inamfanya Doreen kutokwa na damu mdomoni. Nsyuka anaonekana kuibuka kutokea ardhini katika dakika ya 29:19. Halikadhalika, fantasia kama kiunzi cha matukio ya kifilamu inajitokeza wakati Doreen anamkimbia Nsyuka kutoka alikomwacha lakini, kwa ajabu, anamwona amesimama mbele yake. Hii inabainika katika dakika ya 19:04 ya sehemu ya kwanza ya filamu hii. Licha ya Doreen kujaribu kila mbinu ya kumtoroka Nsyuka, bado a anajitokeza mbele yake. Hatimaye, Nsyuka anamkaba Doreen hadi kusababisha mauti yake. Matukio hayo yanakiuka uhalisi kutokana na kubebwa na uajabu mwingi ndani yake. Hali hiyo ya ufantasia ni nadra kuikuta ikijipambanua katika maisha ya kawaida ya wanajamii.

Tukio la pili la kifantasia limejitokeza pindi Sanjo na Daktari Dimoso walipokuwa kwenye teksi lakini, kwa hali ya kushangaza, anatokea Nsyuka mbele yao. Hii inabainika katika dakika ya 40:01 ya seheemu ya tatu ya filamu. Kutokana na Nsyuka kujitokeza kwa ghafla, gari lao linawashinda na kumgonga. Baada ya ajali, wakiwa wamepigwa na butwaa, Nsyuka anajitokeza na kumkamata Sanjo, anamng'ata mkono na kuukata. Tukio hili linabainika katika dakika ya 50:13. Kwa hali ya kutisha zaidi, Nsyuka anaonekana akiutafuna mkono wa Sanjo mithili ya mtu atafunavyo mhindi wa kuchoma. Tukio hili ni la kifantasia kwa sababu halionekani katika maisha ya kawaida.

Tukio la tatu la kifantasia linajitokeza pindi Diana (mchumba wa Daktari Dimoso) alipokuwa akijiandaa kuoga, lakini anatokewa na Nsyuka. Katika tukio hilo linalobainika katika dakika 25:13 ya sehemu ya tatu ya filamu ya *Nsyuka*, Diana anakabwa hadi kuuwawa na Nsyuka.

Tukio la nne la kifantasia linajitokeza pindi Daktari Dimoso na Sanjo walipokuwa wanabishana kuhusu kwenda polisi kuripoti juu ya tukio la Diana kuuwawa na Nsyuka. Wakati wa majadiliano yao, Nsyuka anawatokea na kuwaonya kuwa wasiende polisi. Tukio la tano la kifantasia linajitokeza wakati Scola, Sanjo, na Daktari Dimoso wakiwa wamelala. Doreen anajitokeza kimiujiza akiwa ameshika shada la maua. Anaonekana anamtafuta Sanjo ili amvishe. Tukio hili linabainika katika dakika ya 23:27 ya sehemu ya tatu ya filamu hii. Anamfikia, kisha anamvalisha shada na kumwambia kuwa lazima atakufa kama yeye alivyokufa. Baada ya kusema maneno hayo, anatoweka.

Tukio la sita la kifantasia linajiibua pindi baba yake Daktari Dimoso alipokuwa anamwita mtoto wake. Wakati akiita, Nsyuka anatokea na kutoa kicheko kikali sana. Nsyuka anamsogelea baba huyo na kumkata mguu.

Tukio la saba la kifantasia limejitokeza wakati Daktari Dimoso anapobaini kuwa yupo makaburini na pembeni yake anamwona Nsyuka akicheka huku ameshika mguu wa baba yake. Hili linabainika kuanzia dakika ya 45:05 hadi katika dakika 56:10 ya filamu hii. Kwa vitisho, Nsyuka anang'ata kipande cha mguu huo na kukitafuna.

Tukio la nane la kifantasia linajidhihirisha wakati Scola yupo sebuleni, ghafla, anamuona Doreen ambaye ni marehemu akiwa amekaa kwenye kochi akimwangalia. Doreen anaampa Scola shada la maua lililo katika umbo la msalaba. Anamwambia atalipanda kaburini baada ya kumzika Sanjo.

Tukio la tisa la kifantasia katika filamu ya *Nsyuka* limejitokeza pindi vizuu vinne vinapoonekana nyumbani kwa Scola vikiwa vimembeba Sanjo. Vizuu hivyo vinatokomea na Sanjo mahali kusikojulikana.

Matukio yote haya yaliyobainishwa yanadhihirisha kuwapo kwa hali ya ufantasia katika ujenzi wa filamu za Kiswahili. Matukio ya namna hii yanakiuka uhalisi wa maisha kwani hayaonekani katika mazingira halisi. Kupitia msingi wa kwanza wa Nadharia ya Fantasia, ilibainika kuwa mambo hayo ya kidhahania, licha ya kukiuka uhalisi, yalijengwa mahususi ili kutoa mafunzo kupitia matendo ya wahusika wa filamu.

**Sababu za kutumia ufantasia katika filamu za Kiswahili**

Utafiti uliozaa makala hii ulibaini sababu tano (5) za kutumiwa kwa fantasia katika filamu za Kiswahili. Sababu hizo ni kudhihirisha ubunifu wa msanii,

kujenga taharuki, kuvutia hadhira, kusisimua watoto, na kudhihirisha falsafa ya Kiafrika.

***Kudhihirisha upekee wa kibunifu***

Utafiti uliozaa makala hii ulibaini kuwa fantasia imekuwa ikitumika katika filamu za Kiswahili ili kuupambanua ubunifu na upekee wa msanii katika kazi yake. Halikadhalika, ilibainika kuwa watayarishaji wa filamu wanatumia fantasia ili kuifanya kazi yao iwe tofauti na ya kipekee. Hoja hii inashadidiwa na Mang'ita[1] ambaye anasema:

> Baadhi ya watayarishaji wa filamu za Kiswahili hujikita katika fantasia kwa malengo ya kuleta upekee wa kazi zao. Jambo jingine linalowasukuma kufanya hivi ni kutaka filamu zao ziwe na mvuto unaomtofautisha na watayarishaji wengine. Niseme wazi, mimi ni mpenzi mkubwa wa filamu za kifantasia, hususani za kutisha. Unaweza kushangaa, kwani huwa napenda kutazama filamu hizi nyakati za usiku ...

Bicco[2] anaendelea kuthibitisha hoja kuhusu sababu za watayarishaji wa filamu za Kiswahili kutumia fantasia kwa ajili ya ubunifu na upekee wa filamu. Anasema:

> Fantasia ni muhimu sana kwetu sisi watayarishaji wa filamu. Mbinu hii huwa inatuongezea wigo wa kiubunifu, yaani kuna wakati unakuta kuna fikra fulani ya kibunifu inakusukuma kitu kitakachokuwa cha kipekee, hususani pindi unapotaka kubuni matukio yenye vitu vya kiajabu. Hivyo, utakuta hatuna budi kuibeba fantasia ili itusaidie kufanya kazi zetu ziwe zenye uwasilishaji wa kipekee kututofautisha na watayarishaji wengine.

---

[1] Oliva Eniko Mang'ita ni mwanafunzi wa Shahada ya Umahiri katika Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Mahojiano kati yake na mwandishi wa makala yalifanyika Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma, Septemba 20, 2023.

[2] Mathew Bicco ni mtayarishaji wa filamu za Kiswahili na Katibu Mkuu Mstaafu wa Shirikisho la Filamu nchini Tanzania. Mahojiano haya yalifanyika Sinza Mori, jijini Dar es Salaam, Oktoba 10, 2023.

Dondoo hili linaonesha namna watayarishaji wa filamu wanavyojikita katika fantasia ili kujipa upekee wa kisanii. Isitoshe, ilibainika kuwa wasanii wa filamu za Kiswahili huweka matukio ya ajabuajabu katika kazi zao kama sehemu ya ubunifu. Hali hiyo imekuwa ikileta upekee baina ya kazi moja ya filamu hadi nyingine, hivyo, kuleta mvuto wa kifani katika tasnia ya filamu nchini Tanzania. Utafiti uliozaa makala hii ulibaini kuwapo kwa matukio yaliyofuatana katika ruwaza maalumu katika filamu ya *Nsyuka* yaliyonogesha simulizi ya filamu hiyo. Katika filamu hiyo, mtayarishaji amemtumia mhusika Nsyuka kwa namna ya kipekee kabisa. Hali hiyo imesababisha filamu hiyo iwe tofauti na ya kipekee kifani na kimaudhui.

***Kujenga taharuki***

Ponera (2014) anaeleza kuwa taharuki ni hali ya kuwa na dukuduku la kutaka kujua kuhusu nini kitafuatia katika mfululizo wa usimulizi au utendaji wa kazi ya fasihi. Ilibainika kuwa watayarishaji wa filamu za Kiswahili wamekuwa wakitumia fantasia ili kujenga taharuki na kuamsha shauku kwa hadhira ya kifilamu kutaka kufahamu tukio la kifilamu linalofuatia. Ilibainika kuwa taharuki huweza kujengwa kupitia matumizi ya wahusika wa ajabuajabu wanaotenda matukio ya kiajabu ili kuwatia watazamaji shauku kubwa ya kufuatilia simulizi nzima ya filamu. Jambo hili lilidhihirika katika filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu*, ambapo mtayarishaji wa filamu ametumia fantasia kupitia mhusika Jamila ambaye anasaidiwa kiajabu na pete katika kutimiza majukumu yake. Tumekwishaeleza matukio mbalimbali ya kifantansia kuhusiana na namna pete ya maajabu inavyomsaidia Jamila kutenda kazi zake (kama vile kufagia, kupika, kufua nguo, kumvalisha nguo mpya, kumsafirisha hadi Hifadhi ya Mikumi na kumrejesha nyumbani, na kumwokoa na hila ya

kuuawa na mama yake mlezi). Matukio yote haya huacha bumbuazi kubwa kwa watazamaji, hasa watoto, hivyo, kuwajengea hamu ya kufuatilia simulizi nzima. Kwa ujumla, ilidhihirika kuwa matukio haya yalikuwa yameundwa ili kujenga taharuki kwa mtazamaji wa filamu ili aweze kufuatilia simulizi runingani.

***Kudhihirisha falsafa ya Kiafrika***

Falsafa ya Kiafrika ni kweli za vipengele mbalimbali vya maisha ya Waafrika (Chuachua, 2016). Utafiti ulibaini kuwa watayarishaji wa filamu za Kiswahili wamekuwa wakitumia fantasia ili kudhihirisha falsafa ya Kiafrika. Jamii za Kiafrika huamini masuala ya uganga na usihiri (Mesaki, 1993). Vipengele vya falsafa ya Kiafrika ambavyo vilidhihirika katika filamu teule ni usihiri (uchawi), matambiko, na uganga.

Watayarishaji wa filamu za Kiswahili wamekuwa wakisawiri mdhihiriko wa dhana hizo katika jamii kupitia filamu zao. Katika filamu ya *Nsyuka*, mtayarishaji anaonesha namna Doreen anavyoenda kwa mganga ili apate mtoto. Hata hivyo, anapopewa masharti, anashindwa kuyatimiza kutokana na kuibiwa mkufu uliofungwa dawa. Hali hiyo inasababisha Masu (mtoto aliyepatikana kwa njia za kisihiri) abadilike na kuwa mzuka. Pia, kipengele cha falsafa ya Kiafrika kinadhihirika kupitia Dimoso (mume wa Doreen) anapokimbilia kwa mganga kufanya tambiko ili yeye na familia yake wasisumbuliwe na Nsyuka. Isitoshe, katika filamu ya *Nsyuka,* kuna tukio la uchawi kupitia vizuu vinne vinavyokuja kumbeba Sanjo na kuondoka naye kimaajabu. Kwa upande wa filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu*, mtayarishaji anamtumia mhusika Jamila kama mtu anayelindwa na pete ambayo ni msaada aliopewa na jini.

Kimsingi, ujenzi huu wa fantasia katika matukio ya filamu umeakisi maisha ya Waafrika. Watayarishaji wa filamu ni zao la jamii hivyo wanabuni mambo ambayo yanapatikana katika jamii yao. Hivyo, wamekuwa wakitumia mbinu ya fantasia kutokana na uzoefu wa maisha yao katika jamii. Wakati wakizungumzia jamii yao, hujikuta wakitumia fantasia ili kuipambanua falsafa yao ya Kiafrika. Akikazia jambo hili, Fredrick[3] anasema:

> Mtunzi na mwongozaji wa filamu anakuwa akiyasikia au kuyashuhudia mambo haya ya uchawi na usihiri tangu anazaliwa. Kwa hali hiyo, ni rahisi kwake kujikuta anazungumzia kuhusu majini, mazimwi, vinyamkera, mizuka, na kadhalika kwa kuwa sehemu ya maisha yake ...

Dondoo hilo linathibitisha hoja ya maisha ya Waafrika kufungamana na vipengele vya kifalsafa kama vile uchawi. Haya ni mambo ambayo husikika katika jamii nyingi za Kiafrika, hata kama ni vigumu kuthibitika kisayansi.

***Kusisimua hadhira***

Fantasia ilibainika kutumiwa kwa dhima ya kusisimua hadhira. Kupitia utafiti uliozaa makala hii, iligundulika kuwa watayarishaji wa filamu za Kiswahili wanatumia mbinu hii ili kunogesha kazi zao na kumsisimua mtazamaji pindi atazamapo simulizi ya filamu. Ilibainika kwamba, matukio mengi yenye uajabu katika filamu yalijengwa kwa namna ya kuamsha hisia za mtazamaji. Isitoshe, ili kuzidi kuyatia chuku matukio ya kifantasia na wahusika wake, filamu hizi zinatumia sauti za kutisha kwa dhima ya kumsisimua mtazamaji na kumfanya muda wote awe ametuliza macho yake kwenye filamu. Mathalani, filamu ya *Nsyuka* imesheheni matukio ya

[3] Lucy Fredrick ni shabiki wa filamu za Kiswahili. Mahojiano haya yalifanyika Sinza Vatican, jijini Dar es Salaam, Oktoba 13, 2023.

kutisha ambayo humfanya mtazamaji kutokubandua jicho lake pindi ataizamapo. Akishadidia hoja hii, Mengi[4] anasema:

> Ninachoona, matumizi ya fantasia huchochea uibukaji wa hisia za mtazamaji anapotazama filamu. Mtazamaji wa filamu anapotazama filamu hiyo, husisimka kutokana na matendo mbalimbali yanayoonekana. Kwa mfano, mtazamaji anapotazama filamu ya *Nsyuka*, anasisimka kutokana na matendo ya ajabu yaliyo ndani ya filamu hiyo. Watayarishaji wanatumia mbinu hiyo kwa sababu wanataka kumfikirisha mtazamaji juu ya matendo hayo ...

Kadiri akili ya mtazamaji inavyofikirishwa na matukio ya kifantasia, huzidisha kuvutiwa na kumakinia filamu; hatimaye, hujikuta amefika katika kilele cha hadithi ya filamu.

***Kuvutia watoto kutazama filamu***

Utafiti uliozaa makala hii ulibaini kuwa fantasia imetumika ili kuwavutia watoto kutazama filamu. Jambo hili limedhihirika katika filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu*. Matukio mengi ya filamu hiyo yalijengwa katika hali ya kusadikika. Mbinu hii ilibainika kutumika ili kuwavuta watoto kufuatilia simulizi ya hadithi ya filamu. Watoto wamekuwa wakivutiwa zaidi wanapotazama matukio ya kindoto-ndoto yanayokiuka uhalisi. Kazi nyingi za watoto hujengwa kupitia matukio na hali ya kusadikika (Bakize, 2012; Mutua & Furaha, 2014).

Katika filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu*, tulibaini kuwapo kwa matukio ya ajabuajabu kwa kuwa filamu hiyo iliwalenga watoto na mhusika wake mkuu ni mtoto. Katika kutilia mkazo hoja hii, Adam[5] anasema:

---

[4] Peter Mengi ni shabiki wa filamu za Kiswahili. Mahojiano kati yake na mwandishi wa makala yalifanyika Kisasa, jijini Dodoma, Juni 04, 2023.

[5] Haji Adam ni mtayarishaji wa filamu za Kiswahili. Mahojiano haya yamefanyika Mlimani City, Dar es Salaam, Desemba 13, 2023.

> Katika filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu*, tulitumia matukio ya ajabuajabu kwa sababu aina hii ya filamu shabaha yake ni watoto. Aghalabu, hadithi nyingi za watoto zinakuwa za kusadikika. Inafanyika hivyo kwa sababu ufahamu wa watoto wengi unakuwa katika hali ya kusadikika. Jambo hili huwaongezea watoto ari ya kuwa wadadisi na kuanza kuamsha hisia za kibunifu ...

Dondoo hilo linatujuza sababu zilizotoa msukumo kwa Jamila na pete yake kupatiwa uhusika unaokiuka uhalisi. Kwa jumla, hali hii ya kusadikika ni kichocheo kikubwa kwa watoto kuweza kufungua milango yao ya fahamu na kuwa wadadisi na wabunifu katika kuyatazama masuala mbalimbali yanayowazunguka.

**Athari za kutumia fantasia katika filamu za Kiswahili**

Katika utafiti uliofanyika, imedhihirika kuwa kuna athari za kutumia fantasia katika uundaji wa filamu za Kiswahili. Nazo ni za aina mbili, yaani athari chanya na hasi.

***Faida za kutumia fantasia katika filamu ya Kiswahili***

Faida ya kwanza ya matumizi ya fantasia katika filamu ni kutoa burudani kwa watazamaji. Katika filamu teule zilizotafitiwa, matukio yaliyoundwa na fantasia yanadhihirisha dhima ya kutoa burudani kwa watazamaji wake. Katika filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu*, ni jambo la kuburudisha kuona namna pete ya ajabu inavyomsaidia Jamila kufanya kazi zake. Msingi wa tatu wa Nadharia ya Fantasia unathibitisha jambo hili kwa namna ambayo matendo ya wahusika, ploti, na ufundi wa uchukuaji wa picha jongevu unaibua ishara zinazotamba filamu kwa mvuto na upekee. Fantasia

inayounda matukio hayo katika filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu* inajikita kutoa burudani kwa watoto.

Faida ya pili ya kutumiwa kwa fantasia ni kusaidia kutoa elimu kwa jamii. Kupitia uchunguzi wa filamu teule, ilibainika kuwa matumizi ya fantasia yanatoa mafunzo yanayolengwa kwa hadhira maalumu. Jambo hili linaenda sambamba na msingi wa kwanza wa Nadharia ya Fantasia unaosisitiza kuwa ubunifu wa kidhahania huwa na athari katika usanaji wa mandhari na uteuzi wa wahusika. Mfano mmojawapo wa hoja hii ni pale matumizi ya fantasia yalipotumika kuiasa jamii kuhusu imani potofu. Mathalani, katika filamu ya *Nsyuka*, jamii ilikuwa inaelimishwa kuwa kwenda kwa waganga wa jadi kwa shabaha ya kutafuta watoto si njia salama. Kufanya hivyo kunaepusha masaibu kama yaliyompata Doreen (kupata mtoto aliyekuja kugeuka kuwa mzuka). Katika mfano mwingine, tunaoneshwa katika filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu* kuwa, licha ya mama mlezi wa Jamila kwenda kwa mganga ili asikilizwe na mumewe, anaachika. Elimu inayodhihirishwa hapa ni kuwa maelewano katika ndoa yanajengwa na tabia njema baina ya wanandoa. Suala la kutumia sihiri katika kutatua matatizo ya kimahusiano si suluhu ya changamoto za kindoa.

Faida ya tatu ya kutumiwa kwa fantasia ni kuwajengea watoto tabia njema. Maudhui ya filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu* yanasaidia kuwafahamisha watoto yanayotendeka katika jamii zao. Ni wazi kuwa ufahamu huo unalenga kuwasaidia kuwa wadadisi, kutambua haki zao, kuzisimamia, na kutengeneza hisia za upendo na kuwajali watu wengine.

***Madhara ya kutumia fantasia katika filamu za Kiswahili***

Kupitia utafiti uliozaa makala hii, ilibainika kuwa utumiaji wa fantasia katika usanaji wa filamu za Kiswahili una madhara kwa hadhira. Madhara hayo yamefafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mosi, huifanya jamii kuamini mambo yasiyofaa. Mambo hayo ni kama vile kuamini uganga wa jadi, uchawi na ushirikina. Mathalani, katika filamu ya *Nsyuka*, anaoneshwa Doreen akienda kwa mganga ili kutafuta mtoto. Pia, katika filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu*, Mama Mlezi wa Jamila anakwenda kwa mganga kwa shabaha mbili—kupendwa na mumewe na kumuua Jamila. Tunaona kuwa vitendo hivi vinaweza kuwafanya wanajamii kudhani kuwa kwenda kwa waganga ni suluhu ya kutafuta mafanikio. Hivyo, huweza kuviiga, hatimaye, kuleta taharuki na machafuko ndani ya familia au jamii kwa ujumla. Mathalani, nchini Tanzania kwa miongo kadhaa, kumekuwa na imani potofu kuhusu watu wenye ualbino kuwa viungo vyao vinaleta bahati katika kazi na biashara. Hivyo basi, kutokana na imani hiyo potofu iliyojengeka miongoni mwa jamii, yameshuhudiwa matukio ya kujeruhiwa na kuuwawa kwa watu wenye ualbino.

Pili, ilibainika kuwa fantasia hukengeusha uhalisi wa maisha. Mbinu hii imeonekana kuwa na madhara katika jamii kwa sababu iko kinyume na dhima ya sanaa katika uakisi wa maisha. Kwa mfano, kinachoonekana katika filamu ya *Jamila na Pete ya Ajabu* ni kuwa mtu anaweza kusaidiwa kufanikiwa maishani kwa uwapo wa pete. Katika filamu hiyo, pete ilionekana kumsaidia Jamila kazi na mahitaji kama vile kumpatia chakula, kufua nguo, na kuosha vyombo. Hata hivyo, ni vigumu kwa masuala hayo kutokea katika maisha halisi ya kila siku. Hivyo, kupewa kwake nafasi kunaweza kuchochea uvivu miongoni mwa wanajamii, hususani watoto.

Katika hali halisi ya kijamii, masuala ya kutafuta mali kwa njia za mkato bila kufanya kazi yanaongezeka kila siku. Mathalani, kupitia mambo kisihiri ambayo wakati mwingine wamekuwa wakiyaona katika runinga, wanajamii wamekuwa wakivaa pete za bahati za vito na rangi mbalimbali kwa minajili ya kupata mafanikio ya haraka.

Tatu, matumizi ya mbinu hii, hususani katika filamu, yanajenga hofu kwa watoto. Hali hii husababishwa na matumizi ya wahusika na matukio ya kutisha ambayo watoto hushindwa kuyahimili. Aghalabu, hii huwafanya watoto kuogopa kutembea peke yao, kuweweseka ndotoni, au, nyakati nyingine,, kuogopa kwenda msalani kutokana na mambo ya kutisha waliyoyaona katika filamu. Fajar & Lestari (2021) wanaeleza kuwa, hofu inayojengwa na matukio ya kifantasia inapokomaa akilini mwa watoto, husababisha matatizo ya kisaikolojia, ajali, na vifo. Wanaongeza kuwa woga unaojengwa kwa mtoto hupunguza umakini wake pindi awapo barabarani. Hivyo, anaweza kupata ajali na kusababisha kupoteza maisha.

**Hitimisho**

Makala imedhihirisha matukio mbalimbali yaliyojengwa kifantasia katika filamu teule. Pia, imefafanua sababu za kutumika kwa fantasia katika filamu hizo. Sababu hizo ni: kudhihirisha ubunifu wa msanii, kujenga taharuki, kuvutia hadhira, kusisimua watoto, na kudhihirisha falsafa ya Kiafrika. Vilevile, makala imeeleza faida na madhara ya matumizi ya ufantasia katika katika filamu. Faida zilizobainika ni: kuburudisha, kuelimisha na kuwajengea watoto tabia njema. Madhara yaliyoelezwa ni: kupotosha jamii, kukengeusha uhalisi wa maisha, na kujenga hofu kwa watoto. Ni vema watayarishaji wa filamu wakazingatia uwiano wa matumizi ya fantasia katika filamu. Matukio ya fantasia yaendane na umri, utamaduni, na

mazingira ya hadhira lengwa. Zaidi, vyombo vyenye mamlaka ya kutoa ithibati katika kazi za sanaa kama vile filamu vinatakiwa kuongeza umakini katika kuhakiki matukio ya fantasia kabla ya kuruhusu kazi hizo kwenda kwa hadhira ili kuepusha madhara yaliyoelezwa katika makala hii.

**Marejeleo**

Abdallah. S.A. (2018). *Nafasi ya Fasihi ya Watoto ya Kidijiti katika Kukuza Fasihi Simulizi: Mifano kutoka Vibonzo Jongevu* (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Bakize, L.H. (2012). Fantasia katika Fasihi ya Watoto kwa Watoto. *Kioo cha Lugha*, 10(1), 123-134.

Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya Riwaya za Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Wabantu* (Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Cragan, D.S. & John, F. (1995). *Symbolic Theories in Applied Communication*. New Jersey: Hampton Press.

Fajar, R. & Lestari, T. (2021). The Influence of Horror Films on Personality Development and Emotional Children. *Journal of Gender and Child Studies*, 5(1), 17-26.

Hamad, A.H. (2019). *Dhima za Taharuki katika Riwaya za Kiswahili* (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). State University of Zanzibar, Unguja.

Hunt, P. (Ed). (1990). *Children's Literature: The Development of Criticism*. London: Routledge.

Kasiga, G.A. (2024). Tathmini ya Muziki wa Kizazi Kipya Karne ya 21 Nchini Tanzania: Tija na Madhara Yake. *Mulika*, 42(1): 66-82.

Kasiga, G.A. (2022). *Tathimini ya U-Nigeria katika Video za Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya wa Kiswahili Nchini Tanzania* (Tasinifu ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Kasiga, G.A. (2019). Mwanzo na Mdhihiriko wa U-Nigeria katika Filamu za Kiswahili. Katika, A.S. Ponera & Z.A. Badru (Wahariri). *Koja la Taaluma za Insia*: *Kwa Heshima ya Profesa Joshua Madumulla* (663-680). Dar es Salaam: Karljamer Publisher Limited.

Kasiga, G.A. (2018). U-Nigeria: Athari zake katika Filamu za Kiswahili. *Mulika*, 37: 72-84.

Kasiga, G.A. (2013). *U-Nigeria katika Filamu za Ki-Tanzania* (Tasinifu ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Kasiga, G.A. & Luhwago, N. (2020). Filamu ya Kiswahili: Fasihi Simulizi Iliyostawi. *Mwanga wa Lugha* 5(1), 107-124.

Kasiga, G.A. & Maffa, M.M. (2021). Dhima ya Sadfa ya Kimapenzi katika Kujenga Matukio ya 'Kishushushu' na 'Kijasusi': Uchunguzi wa Riwaya ya Kikosi cha Kisasi. *Mulika*, 40(2): 109-123.

Mahenge, E. (2016). *Drama za Kiswahili*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Mesaki, S. (1993). *Witchcraft and Witch-killings in Tanzania: Paradox and Dillema* (Tasinifu ya Uzamivu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Minnesota, Minnesota.

Mutua, J.M. & Furaha, C. (2014). Fani za Fasihi Zinazoibua Fantasia katika Hadithi za Watoto za Nyambura Mpesha. *Nordic Journal of African Studies*, 23(4): 292-306.

Mrikaria, S.E. (2007). Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya. *Swahili Forum*, 14: 197-206.

Ponera, A.S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.

Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Ponera, A.S. & Kasiga, G.A. (2019). Mdhihiriko wa Kionjo cha Usangwini kwa Mhusika Willy Gamba katika Riwaya ya Njama. *Kioo cha Lugha*, 17: 99-113.

Sadner, D. (1996). *Literature for Children and Young People in Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Suwed, A.A. (2013). *Usawiri wa Ujinsia katika Filamu: Uchunguzi wa Matumizi ya Lugha katika Filamu za Steven Kanumba* (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

Walibora, K.W. (2010). Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe: Mshabaha kati ya *Dunia Yao* na *The Tin Drum*. *Swahili Forum*, 17: 143-157.

Wamitila, K.W. (2013). Mikakati ya Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili. *Mulika*, 32: 1-12.

Yangi, E. (2015). *Matumizi ya Tamathali za Semi katika Nyimbo za Misiba kwa Jamii ya Wahehe* (Tasinifu ya Umahiri, Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.